

Ushiriki wa Ndugu katika Olimpiki Maalum

Ushiriki wa ndugu hutokea ambapo ndugu wa mtu aliye na ulemavu wa akili anashiriki kikamilifu katika maisha ya ndugu au dadake. Ndugu wanaojihusisha ni washiriki wanaoshiriki kikamilifu katika safari za Olimpiki Maalum za kaka na dada zao. Huwa wanacheza, kujifunza, kukua na kufanya kazi kwa pamoja, wakiimarisha uhusiano wao katika hizo harakati. Ndugu hao ni timu ambayo hutiana motisha na kutegemeana. Wanajitahidi ili kufikia malengo yao ya pamoja na kibinafsi.

Kuna njia nyingi ambazo unaweza kuwa ndugu anayejihusisha katika Olimpiki Maalum, ikiwa ni pamoja na:

Kusaidia

- Kumshangilia ndugu yako

Kushiriki

- Wanamichezo Wachanga
- Michezo Iliyunganishwa
- Ushiriki katika Vyuo Vikuu
- Kuwa mkufunzi wa Olimpiki Maalum

Kupata uhodari

- Unified Fitness Club
- Familia Hodari
- SOfit

Kujitolea

- Kujitolea katika Matukio ya Olimpiki Maalum
- Wachezaji walio na Afya
- Kuwa Ofisa wa Olimpiki Maalum

Kuunganisha

- Mtandao wa Usaidizi kwa Familia

Utetezi

- Kutetea Shule Nzima
- Uongozi wa Vijana Unaojumuisha
- Uongozi wa Mipango

Ushiriki wa Ndugu kupitia Olimpiki Maalum ina **matokeo yenye kuwanufaisha** wewe na ndugu yako. Ndugu yako atathamini muda unaochukua kuwekeza katika malengo yake.

Ushiriki wa ndugu kunaweza kukakupa:

- Kujivunia kwako na kwa ndugu yako
- Ongezeko la kujistahi
- Ujuzi wa ukuzaji wa taaluma
- Ujuzi wa uongozi na fursa
- Ujuzi wa uteteaji
- Urafiki na ndugu na wanamichezo wengine
- Uhusiano wa karibu zaidi na ndugu yako
- Uvumilivu zaidi na kuwakubali watu wote
- Umoja wenye nguvu zaidi katika familia
- Fursa za kukua kibinafsi na kimichezo

Kama ndugu, kuna njia nyingi ambazo unawezashiriki katika Olimpiki Maalum maishani mwako. Jukumu lako katika Olimpiki Maalum litabadilika kwa muda kulingana na unayoyapenda, malengo yako na muda ulioratibu kutumia.

Huwa kuna haja ya watu wa kujitolea wakati wote katika Olimpiki Maalum.

Kwa habari zaidi kuhusu ushiriki wa ndugu katika Olimpiki Maalum, angalia [Mwongozo wa Ushiriki wa Ndugu wa Vijana!](#)

